

Pastor James Kalekwa

# KAZI YA MUNGU NI KAZI

## MAENEO 6 YA KIMAANDALIZI KWA MTUMISHI KIJANA

# KAZI YA MUNGU NI KAZI…

*Maeneo 6 ya kimaandalizi kwa mtumishi kijana.*

James Kalekwa

## Orodha ya Yaliyomo

**Tabaruku** ........................................ 4

**Salamu na Utangulizi** ........................................ 5

ULAZIMA WA MAANDALIZI YA UTUMISHI KWA MTUMISHI KIJANA. ........................................ 7

MAANDALIZI YA KIROHO ........................................ 13

MAANDALIZI YA KIMTAZAMO ........................................ 23

MAANDALIZI YA KIWITO ........................................ 42

MAANDALIZI YA KIMAONO ........................................ 44

MANDALIZI YA KIMAARIFA ........................................ 54

MAANDALIZI YA KIMWILI ........................................ 59

**Kuhusu Mwandishi:** ........................................ 61

**Kuhusu New Vine Church:** ........................................ 61

**Mawasiliano na Mwandishi:** ........................................ 62

## Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

## Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake **Juni 20**, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anavyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani

huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2024
Dodoma, Tanzania

# ULAZIMA WA MAANDALIZI YA UTUMISHI KWA MTUMISHI KIJANA.

Ukiwa unasafiri kutoka Dodoma mjini kwenda wilaya nyingine ya mkoa wa Dodoma na ukawa umekusudia kurejea mjini siku hiyo hiyo, kuna aina ya maandalizi utakuwa nayo. Iwapo utasafiri nje ya mkoa wa Dodoma kwenda mkoa mwingine, kuna kiwango na aina ya maandalizi yataonekana… kifedha, kimavazi, mpangilio wa muda wa safari na mambo yanayofanana na hayo. Ikiwa unasafiri kutoka Dodoma kwenda nje ya nchi, kutakuwa na aina tofauti ya kimaandalizi. Hapa utahitaji hati ya kusafiria na nyaraka nyinginezo za kiafya au uhamiaji kulingana na matakwa ya taifa unaloenda.

Kwa mfano, unatoka Dodoma kwenda mji wa Tampere, Finland (Ulaya Kaskazini). Utagundua ya kwamba maandalizi ya safari yanaweza kukutaka miezi hata sita kabla ya safari. Wakati safari ya ndani ya mkoa wa Dodoma inaweza kuandaliwa ndani ya dakika kumi tu na ikatekelezwa. Gharama zinazoambatana na safari; nidhamu ya safari; uelewa kuhusu muda, fedha

(currency), hali ya hewa na tamaduni ni jambo la kuzingatiwa kulingana na umbali wa safari. Kwa kadiri safari inavyokuwa ya mbali na muda mrefu ndivyo ambavyo inagharimu zaidi kwenye maandalizi. Huwezi kwenda ulaya kwa kutumia gharama za Bahi!

Kwa mfano huo ninataka tuutazame utumishi na kazi ya Mungu kwa ujumla wake. Uelewa wetu kuhusu ukubwa, umbali na uzito wa safari hii utaamua sana uhitaji na uwekezaji wetu kwenye maandalizi na hatimaye ni kwa namna gani tunaiendea kazi ya Mungu.

Kwenye mapokeo (traditions) ya hapa kwetu Tanzania, walau kwenye makanisa ya kihistoria, kwa nyakati hizo. Ilionekana utumishi kuwa ni chaguo la mwisho ambalo kijana hushauriwa na wazazi wake kuliendea baada ya kila jambo la kielimu au kimaisha kuwa limeshindikana. Nimewahi kushuhudia zaidi ya mara moja, kijana baada ya kumaliza elimu ya upili, amejaribu kuomba nafasi kadhaa kulingana na kiwango cha ufaulu wake bila mafanikio. Baada ya hayo yote, wazazi wake walimshauri, *"…kasomee uinjilisti sasa…"*. Sasa, kwa muktadha wa kanisa alilokuwamo, hiyo ilimaanisha

kuingia katika utumishi rasmi wa kanisa. Ngazi ya kuingilia ni kujisali kwenye mafunzo yatolewayo na mfumo wa kanisa husika.

Kwenye makanisa ya kikarismatiki, shuhuda nyingi za kuingia kwenye kazi ya Mungu ni zile za kuona kila kitu hakiendi, kila mlango umefunga, kila kitu unachotia mkono kukitenda hakisogei… unathibitisha ya kuwa, *"nimeitwa na Bwana".* Labda kwa sasa, simulizi imegeuka kidogo… watumishi wanavutiwa na uwasilishaji wa nje na kimwonekanao wa utumishi unaofanywa na watumishi waliotangulia kiasi cha kuufanya utumishi kuvutia.

Vyovyote vile, swali langu kubwa Je, unaifahamu hii safari? Unaujua umbali wa safari hii? Hivi kweli umeandaliwa na/au umejindaa kuiendea safari hii.

Uelewa unaowasilishwa kwa njia ya neno la Mungu unaonyesha ya kwamba utumishi ni kazi… tena ni kazi haswa! Mifano inayotumika kuulezea utumishi inaonyesha ya kwamba si eneo la watu wavivu au walegevu. Ni kazi inayokula muda, nguvu, akili, hisia,

nidhamu… utumishi utagharimu maisha yako yote ili uufanye.

Kwenye sura hii ninakuwasilishia taswira kadhaa ambazo utumishi unatajwa nazo. Hii itakusaidia kuuweka utumishi mahali unapopaswa kuwa (putting it into perspective).

2 Tim 2:3-7 SUV *"[3] Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. [4] Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari. [5] Hata mtu akishindana katika machezo hapewi taji, asiposhindana kwa halali. [6] Yampasa mkulima mwenye taabu ya kazi kuwa wa kwanza wa kupata fungu la matunda. [7] Yafahamu sana hayo nisemayo, kwa maana Bwana atakupa akili katika mambo yote."*

1 Kor 3:9 SUV, *"[9] Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu."*

1 Kor 9:7 SUV, *“[7] Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?”*

Mfananisho wa huduma/utumishi anaoutumia Mtume Paulo unatengeneza ulazima wa kuhitaji maandalizi kwa yeyote anayetaka kuingia kwenye huduma.

1. Vita/Mapigano
2. Michezo
3. Kilimo/Shamba
4. Ujenzi wa nyumba/jengo
5. Uchungaji wa kundi la mifugo

Note: Yafahamu sana hayo ayasemayo – yapi? Hizo “*allegories*” zinazohusu utumishi. Ukizifahamu hizo ndiyo Mungu anakupa akili kwenye mambo yote.

Usipoyafahamu hayo, utakuwa ni mtumishi mwenye wito na upako lakini usiye na akili katika mambo yote.

Hiyo mifano mitano (allegories), zinapendekeza kwamba huduma ni kazi ngumu (labour) inayotaka nidhamu ya hali ya juu sana. Ambayo itakutaka kila kitu ili kuitimiliza... chunguza hizo fani kama zinavutia wavivu.

# MAANDALIZI YA KIROHO

Utumishi ni kazi ya kiroho. Ichukulie hivyo na uitende hivyo. Usifanye utumishi kimwili.

Moja ya kazi za ajabu sana duniani ni utumishi huu kwa Mungu wetu. Unamtumikia mwajiri ambaye ni wa kiroho (spiritual entity) na taratibu zake ni za kiroho. Hata hivyo, utekelezaji wa utumishi huu ni kwenye ulimwengu wa mwili kwa wanadamu – wanufaika wa utumishi. Namna ya kuendesha utumishi huu inapaswa kuwa ya kiroho. Thawabu na ujira wake ni vya kiroho.

Utambuzi huu tu unaita na kulazimisha maandalizi makubwa ya kiroho kwa uendelevu.

i. Okoka – Mungu anajali sana mahusiano binafsi juu ya mahusiano ya kazi. Si kwamba hajali wewe kuwa mtumishi wake, bali ninazungumzia vipaumbele hapa.

Ninajua kimoyomoyo ni kama unataka kuaruka hapa uende maeneo mengine ya maana. Ukweli hili ndilo eneo la maana sana kuliko sehemu yoyote ya kitabu hiki.

Si tu mimi ninasema, lakini kwa mifano ya Bwana Yesu na maneno ya mitume kuna pendekezo ya kwamba inawezekana kumtumikia Mungu bila kuwa na mahusiano binafsi – bila kuokoka. Hebu tazama kile ambacho Bwana Yesu anakisema:

*"Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? 23Ndipo nitawaambia dhahiri, **Sikuwajua ninyi kamwe**; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu."* Mathayo 7:22-23

Hoja hii huwa inanishangaza sana. Hao ndugu watasema juu ya utumishi wao. Bwana Yesu hatakanusha kuhusu utumishi wao. Ajabu na kweli walitumia jina la Bwana Yesu mwenyewe kwenye utendaji wao wa kimaajabu. Jambo linalonionyesha uendelevu wa wazo la Bwana Yesu (consistency in pattern of thinking). Wale ndugu ndiyo wanasema walitenda miujiza na kutoa pepo, siyo Bwana Yesu! Jibu la Bwana Yesu ni moja tu, "sikuwajua ninyi kamwe!" maana yake siyo siwajui leo, bali siwajui hata siku mlipokuwa mnafanya utumishi.

Je, kuna uwezekano hata kumbe walikuwa hawatoi pepo na kutenda ishara na miujiza kwa tafsiri ya Bwana Yesu? Ni jambo la kufikirisha sana.

Mtume Paulo mwenyewe anazungumza kumuhusu yeye mwenyewe, *"bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe,* ***nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.****"* 1 Kor 9:27… Subiri! Kumbe kuna uwezekano wa kukataliwa baada ya kuwahubiri wengine?

Hii inatukumbusha ya kwamba kabla ya kukimbilia kuwahubiri wengine, kutoa pepo, kutenda miujiza na ishara… kwanza hakikisha una mahusiano binafsi na Bwana Yesu.

ii. Kulia wokovu – (Maliza mafundisho ya awali/mafundisho ya msingi ya imani kabla hujaenda kwenye huduma)

Ili mtu afike mahali pa kuanza kufundisha wengine ni sharti awe kwanza amefundishwa na kuhitimu maundisho ya awali na kuyakulia. Moja ya jambo lililokuwa linamkera mwandishi wa Waebrania ni kwa namna gani wasomaji wake "wamegoma" kuukulia

wokovu. Bado wanarudishwa wenye mafundisho ya awali ya wokovu wakati walipaswa kuwa walimu wa wengine. Ukiweka uwiano wa muda ndani ya wokovu ikilinganishwa na mwitikio wao wa kiukuaji kwenye mafundisho.

*"Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake; na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia. 12Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. 13Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. 14Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya."* Waebrani 5:11-14

*"Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu; tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu, 2na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na*

*hukumu ya milele. 3Na hayo tutafanya Mungu akitujalia."* Waebrania 6:1-4

iii. Ukomavu wa kiroho - 1 Kor 3:1-3 (Watoto, Tabia ya mwilini na Mtu wa tabia ya rohoni).

Nikuambie jambo ambalo nitakushauri uruhusu liingie rohoni mwako na si kwenye masikio yako tu: Huduma si kwa ajili ya watoto wachanga na watu wa tabia ya mwilini.

*"Lakini, ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama na watu wenye tabia ya rohoni, bali kama na watu wenye tabia ya mwilini, kama na watoto wachanga katika Kristo. 2Naliwanywesha maziwa sikuwalisha chakula; kwa kuwa mlikuwa hamjakiweza. Naam, hata sasa hamkiwezi, 3kwa maana hata sasa ninyi ni watu wa tabia ya mwilini. Maana, ikiwa kwenu kuna husuda na fitina, je! Si watu wa tabia ya mwilini ninyi; tena mnaenenda kwa jinsi ya kibinadamu?"* 1 Wakorintho 3:1-3

*"Wala* ***asiwe mtu aliyeongoka karibu****, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi."* 1 Timotheo 3:

iv. Ufunikwe katika maombi – (Mf: Maombi ya kujiweka wakfu/kujidhabihu); Maombi ya vita na mapigano.

Moja ya jambo linalokosekana sasa kwenye mwili wa Kristo ni ule muundo wa kanisa la mwanzo. Watumishi wa injili walizingirwa na wigo wa maombi kila mji na kila pande na jumuiya kubwa ya waamini. Utagundua mojawapo ya jambo linalojitokeza kwa uendelevu kwenye nyaraka za Mtume Paulo, ukiondoa salamu na namna yake ya upekee ya kufunga barua… ni hili swala la uhitaji wa yeye mtume kufunikwa maombini na jumuiya ya waamini.

Mtazamo wa wengi kwa sasa ni kwamba mtumishi ni kinara ambaye yuko mahali fulani kisha watu wengine wote wanamkusanyikia ili kuombewa. Usiingie kwenye huo mtego wa kuwa kinara au mtumishi mashuhuri. Ninajua hili si wazo maarufu (popular opinion) bali ni wazo la Kibiblia. Kwa kuwa hii ndiyo njia iliyomfaniskisha mtume Paulo kwenye utendaji wake wa huduma, basi ni njia ya uhakika kuifuata.

Hata hivyo kwa kufundisha hivyo simaanishi ukasimishe maisha yako binafsi na jukumu lako binafsi la kuomba… HAPANA! Usininukuu vibaya.

*“wa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;* ***pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya Injili****;”* Waefeso 6:18-19

*“Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika kuomba huku na shukrani;* ***mkituombea na sisi pia, kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo,*** *ambayo kwa ajili yake nimefungwa, ili niidhihirishe, kama inipasavyo kunena.”* Wakolosai 4:2-4

v. Karama za Roho na Utendaji wake

Karama ni nyenzo mikononi mwa mtumishi kwa ajili ya kuwezesha utendaji wa kazi ya Mungu. Haiwezekani kumtumikia Mungu bila karama kuingia kazini. Kwa sababu kimsingi, karama za rohoni ndiyo vifaa vya kiroho. Usisahau hili, kazi ya Mungu ni kazi ya kiroho.

Nitakuwekea maandiko kadhaa hapa kwanza ili kuzalisha ufahamu ndani yako kuhusu karama za rohoni; pili, ili kuzalisha shauku ndani yako kuhusiana na karama na utendaji wake kwenye maisha ya kazi ya Mungu.

*"**Takeni sana karama zilizo kuu**. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora."* 1 Kor 12:31

*"Basi, ndugu zangu, **kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu.**"* 1 Kor 12:1

*"Ufuateni upendo, **na kutaka sana karama za rohoni**, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu."* 1 Kor 14:1

*"Kwa sababu hiyo nakukumbusha, **uichochee karama ya Mungu**, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu."* 2 Timotheo 1:6

*"**Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako**, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee."* 1 Tim 4:14

Mtu asiyetenda kazi ya Mungu kwa kuwezesha na karama basi uwezekano ni mkubwa sana kwamba

hatendi kazi ya Mungu. Ukweli wa mambo ni kwamba, pasipo uwezesho wa kiungu huwezi kuitenda kazi ya Mungu. Ina taarifa nyingi na mawanda mapana (it has a lot of details and dynamics). Kiasi kwamba akili ya mwanadamu haiwezi kuibeba na kuistahimili.

*"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana;* ***maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote****."* Yohana 15:5

Kwenye muktadha wa awali wa andiko anamaanisha pasipo mimi, ninyi hamuwezi "kuzaa matunda ya zabibu", yaani, hamuwezi kuwa na matokeo. Tawi linalojitegemea kuzaa, ni tawi ambao halitakuja kuzaa kamwe.

Sababu ya pili ya maandalizi kwenye eneo hili ni kwamba, Mungu amekusudia utendaji wa kazi yake kubwa na ya kutisha ufanywe na watu *"wanyonge"* kwa vipimo vya dunia hii ili ijulikane ni Mungu anayetenda na siyo vigezo vya chombo husika. Nitakuwekea maandiko kadhaa hapa ili uweze kuona na kutafakri mwenyewe:

*"Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, **kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga**."* Mathayo 11:25

*"Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba **si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa**; bali Mungu aliyachagua **mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa,** naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; mwenye mwili awaye yote asije akajisifu mbele za Mungu."* 1 Kor 1:26-29

Ukweli ni kwamba, ile tu Yesu amenichagua ni ishara ya kwamba kwa vipimo vya dunia hii mimi ni mpumbavu, dhaifu na mnyonge. Sasa kutaka kujitutumua na kujionyesha ya kuwa mimi nina nguvu zangu mwenyewe na kutumia hizo kuifanya kazi ya Mungu ni kiwango cha juu sana cha upumbavu!

# MAANDALIZI YA KIMTAZAMO

Kuna aina ya uelewa unapaswa kuukubali na kuumiliki ili uwe na tija kwenye utumishi... Mtazamo wako unaamua kila kitu. Ninapozungumzia mtazamo hapa ninamaanisha namna unavyopokea; unavyochakata; namna unavyotafsiri; na namna unavyofanyia maamuzi na kutendea kazi. Kuna mfano mmoja huwa ninapenda kuutumia linapokuja swala la mtazamo. Fikiria mtu aliyevaa miwani ya rangi nyeusi. Hata kama ni mchana kweupe hali huanza kuonekana kuwa ni kama giza. Inategemea sana uelewa alionao kuhusu giza huchochea matendo gani… kuna wanaume neno giza humaanisha ruhusa ya kujisaidia haja ndogo mahali popote pale.

Mtazamo ni mkusanyiko wa uelewa, uzoefu, hisia, ujuzi, elimu na mambo kama hayo. Hivyo huwa ndani ya mtu kumuwezesha kuyaendea maisha. Ni kama miwani inayomsaidia kuiona dunia. Kwenye lugha ya kiingereza hutumika neno *“worldview”* – mahali mtu analiposimama ili kuiona dunia.

Mit 23:7 SUV, *"[7] Maana **aonavyo nafsini mwake**, ndivyo alivyo. Akuambia, Haya, kula, kunywa; Lakini moyo wake hauwi pamoja nawe."*

Kama kuna swali nitakuuliza muda mwingi kwa uendelevu ni hili: Kwani wewe unafahamu nini kuhusu huduma? Kwani wewe unaonaje huduma?

Kuna mitazamo kadhaa inaainishwa kwenye maandiko Mtakatifu kuhusiana na huduma. Kuna watu ambao walikuwa na namna wanaitazama na kuiendea huduma. Ninakuwasilishia mitazamo baadhi kuwezesha tafakari yako:

*"Wengine wanahubiri habari za Kristo kwa sababu ya husuda na fitina; na wengine kwa nia njema. **Hawa wanamhubiri kwa pendo**, wakijua ya kuwa nimewekwa ili niitetee Injili; **bali wengine** wanamhubiri Kristo kwa fitina, wala si kwa moyo mweupe, wakidhani kuongeza dhiki za kufungwa kwangu."* Wafilipi 1:15-17

Umeyaona hayo makundi mawili ya wahubiri? ***Hawa*** na ***wengine.*** Wote wanahubiri, ni sawa! Lakini malengo ya kuhubiri ni tofauti. Kundi la "Hawa" linahubiri injili ili

ienee. Ni kama wanafidishia upungufu *"sokoni"* kwa kumkosa Paulo, Mtume. Hali ya mioyo yao wanapoiendea injili ni hali ya pendo. Kwa upande mwingine wa shilingi, kuna kundi la "wengine" ambalo lengo lake katika kuhubiri ni kuongeza dhiki ya kufungwa kwa Paulo, Mtume. Kundi hili lilikuwa na wivu mkubwa dhidi ya utume wa Paulo na utendaji wake wa huduma, uelewa wake juu ya ufunuo wa Kristo hasa miongoni mwa mataifa. Wao walitafsiri kuwa Paulo ni maarufu, mwenye kusifiwa, kupokelewa vyema na mataifa. Hivyo basi, kipindi akiwa kwenye vifungo ilikuwa ni wakati muafaka "kuiba" mioyo ya watu. Kujitafutia umaarufu na heshima inayoambatana na utumishi. Huenda Paulo akitoka gerezani akute watu wote wamewageukia na kuwafuata watu hawa.

Ni dhahairi ungeona hali ya mashindano kwa watu hawa. Hiyo inaathiri namna ya uwasilishaji wa injili.

Ukisoma kwa jicho hili la mtazamo kuhusu injili na utumishi kwenye nyaraka za Paulo, utaona akitaja baadhi ya makudi ya watu ambao walipita kwenye makanisa baada ya yeye kupita na kufanya huduma. Makundi hayo

yalikuwa na aina fulani ya mtazamo ulioiumiza injili na utendaji wa huduma kwa ujumla wake.

Kwenye kitabu cha Wagalatia, kuna kundi linapita na mtazamo wa dini ya Kiyahudi na mapokeo. Linaenda mbali mpaka kuwataka waamini wapya kupitia michakato ya Kiyahudi kama vile tohara ili kuhesabiwa haki (tohara inaweza kufanya kutokea kwenye mtazamo wa kiafya ni sawa… lakini si mtazamo wa kiinjili).

*"Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo."* **Wagalatia 1:6-7**

*"Lakini Tito aliyekuwa pamoja nami, naye ni Myunani, hakulazimishwa kutahiriwa. Bali kwa ajili ya ndugu za uongo walioingizwa kwa siri; ambao waliingia kwa siri ili kuupeleleza uhuru wetu tulio nao katika Kristo Yesu, ili watutie utumwani;"* **Wagalatia 2:3-4**

Kwenye kanisa la Korintho kulitokea kundi la "mitume" waliohoji uhalali wa utume wa Paulo, mamlaka yake ya kitume na hata mafundisho yake. Wakaenda mbali mpaka kumdhihaki kuhusu hulka zake – ni mtu mkali awapo mbali na ni mtu mlaini sana awapo karibu na Korintho. Kwa hiyo, ili kushindana na Paulo wanaibuka na mafundisho mapotofu na kutafuta kipato kwa nguvu kutoka kwa kanisa hilo.

Ninakuambatanishia maandiko kadhaa hapa. Ili kukusaidia kufuata mtiririko wa wazo ninalowasilisha kwenye sura hii nitaweka mikazo kwenye maneno fulani ili yakusaidie kunasa ninachokiwasilisha.

*"Lakini nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo. Maana yeye ajaye* ***akihubiri Yesu mwingine*** *ambaye sisi hatukumhubiri, au* ***mkipokea roho nyingine*** *msiyoipokea, au* ***injili nyingine*** *msiyoikubali, mnatenda vema kuvumiliana naye!"* **2 Korintho 11:3-4**

*"Je! Nalifanya dhambi kwa kunyenyekea ili ninyi mtukuzwe,* ***kwa sababu naliwahubiri Injili ya Mungu bila ujira****? Naliwanyang'anya makanisa mengine mali yao, nikitwaa posho langu ili niwahudumie ninyi. Nami nilipokuwa pamoja nanyi na kuhitaji sikumlemea mtu. Maana hao ndugu waliokuja kutoka Makedonia walinipa kadiri ya mahitaji yangu; nami katika mambo yote najilinda nafsi yangu nisiwalemee hata kidogo; tena najilinda."* **2 Korintho 11:7-9**

*"Maana* ***watu kama hao ni mitume wa uongo****, watendao kazi kwa hila,* ***wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo.*** *Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao."* **2 Korintho 11:13-15**

Unaona hitimisho la mtume Paulo? Anaita hilo kundi kuwa ni mtiume wa uongo. Halafu haiachi sentensi ibakie hewani yenyewe bali anatoa tasfiri, *"watendao kazi kwa hila"*. Hila ni uwasilishaji unaotofautiana na nia ya ndani. Yaani kile kinachoonyeshwa kwa nje siyo

kilichokusudiwa kwa ndani. Kwa lugha rahisi, ni pale ambapo "shetani" husema ukweli… kwa lengo la kudanganya! Kwenye falsafa na ujenzi wa hoja zenye mantiki, kuna kitu huitwa *"premises"* (hoja zinazotangulia ili kujenga) kisha huwa kuna *"conclusions"* (Hitimisho la hoja kutokana na hoja zilizotangulia). Adui husema ukweli tu pale anapotaka kufikia hitimisho la uongo. Hiyo ndiyo maana halisi ya hila.

Jambo linalovuta sana umakini wangu ni kwamba wahudumu hawa wanaweza "kujigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo." Kumbe inawezekana!

Sasa, usisahau tunakotokea… mtazamo wao kuhusu huduma.

Kwenye kanisa la Thesalonike, kulitokea kundi la wahubiri lililoenda kuhubiri kinyume na mafundisho ya mtume kwa kupotosha. Kimsingi, hawa walienda na mafundisho yenye mikazo iliyopitiliza (extrimism) kwenye maeneo fulani fulani ya imani. Walikazia ya kwamba Yesu Kristo atarudi punde si punde. Hii ni

kutokana na kanisa kutokuelewa kile mtume Paulo alichokifundisha kuhusu siku ya kuja kwa Bwana Yesu. Wengine walidhani imewadia na wengine walitafsiri ya kuwa siku hiyo imeshaanza kutokea. Hivyo, waamini ndani ya kanisa wanapaswa kukaa mkao wa kuondoa. Fundisho hili lilipelekea hali ya uzembe na kutowajibika kwa kufanya kazi za mikono miongoni mwa waamini ndani ya kanisa.

*"Basi, ndugu, tunakusihini, **kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake**, kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu, wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala **kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu**, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo. **Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yo yote**; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu; akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu;"* 2 Thesalonike 2:1-3

Sasa, fuata mtiririko wa wazo analolifundisha Paulo kama madhara ya mikazo iliyopitiliza kutoka kwenye waraka wa unaodhaniwa kuwa ni wa Paulo (na wenzake). Imepelekea hali ya kwenda nje ya utaratibu na

kutokufanya kazi miongoni mwa jamaa ya waaminio. Jambo ambalo mtume analiinukia kwa nguvu na kulikemea kwa uwezo mkubwa sana.

*"Ndugu, twawaagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo,* ***jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu****, wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu. Mwajua wenyewe jinsi iwapasavyo kutufuata; kwa sababu hatukuenda bila utaratibu kwenu; wala hatukula chakula kwa mtu ye yote bure;* ***bali kwa taabu na masumbufu, usiku na mchana tulitenda kazi****, ili tusimlemee mtu wa kwenu awaye yote. Si kwamba hatuna amri, lakini makusudi tufanye nafsi zetu kuwa kielelezo kwenu, mtufuate. Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili,* ***kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula.*** *Maana twasikia kwamba* ***wako watu kwenu waendao bila utaratibu, hawana shughuli zao wenyewe, lakini wanajishughulisha na mambo ya wengine.*** *Basi twawaagiza hao, na kuwaonya katika Bwana Yesu Kristo,* ***watende kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe.*** *Lakini ninyi, ndugu, msikate tamaa katika*

*kutenda mema. Na ikiwa mtu awaye yote halishiki neno letu la waraka huu, jihadharini na mtu huyo, wala msizungumze naye, apate kutahayari; lakini msimhesabu kuwa adui, bali mwonyeni kama ndugu."* **2 Thesalonike 3:6-15**

Umeona kwa jinsi ambavyo kuanzia kanisa la mwanzo swala la mtazamo lilikuwa ni nyeti sana kwa mitume na wahudumu wa injili? Umegundua ya kwamba mtazamo wako unaweza kukupelekea kuwa mtu wa hila, kutafuta umaarufu, mapato kiasi cha kufundisha hata mapotofu? Umengua ya kuwa mtazamo unaweza ukakupelekea hata kuanza kuzalisha nyaraka/machapisho ya uongo na upotoshaji? Umegundua ya kuwa mtazamo wako unaweza ukakupeleka kuanza kuwapinga na kuwapiga vita watumishi wenzako ambao kimsingi ni ndugu zako na wajenzi pamoja na wewe kwenye ufalme wa Mungu? Umegundua ya kwamba mtazamo ni kila kitu?

Kuna mambo kadhaa ya kimtazamo ninayawasilisha kwako ili uweze kutafakari na kuona ni kwa namna gani unajiandaa na kujenga mtazamo sahihi:

i. Kazi kuu.

Utuishi ni kazi ya heshima (noble work). Ni kazi kuu. Ni ajira kwenye mamlaka kubwa kuliko zote mbinguni na duniani. Unatumika kwenye ofisi yenye rasilimali zote; ofisi yenye majeshi yote; ofisi yenye nguvu kuliko yeyote!

Umewahi kusikia watu wanaofanyakazi kwenye taasisi fulani za kidunia – ama serikalini au mashirika binafsi? Labda ofisi za Umoja wa Mataifa? Umewahi kusikia namna watu wanaotumika kwenye fani fulani zinazochukuliwa kuwa za heshima hapa duniani?

Kuna watu hujitambulisha kabla ya kuulizwa; wengine hiupenda kuvaa sare au mwonekano unaotambulisha ofisi zao.

Mtumishi, usikae kinyonge wala kwenye hali ya kuhurumisha. Wewe unafanya kazi na ofisi kuu.

Ni vyema ukajua, hatimaye, watu wote wenye hadhi, nafasi na namna mbalimbali wanamuhitaji kiongozi wa kiroho kuwapa majibu yaliyo juu ya upeo wao – mambo ya ulimwengu wa roho na tafsiri yake kweye ulimwengu

wa mwili na maisha ya siku kwa siku. Macho yote yanakuelekea wewe!

ii. Kazi ngumu (siyo kwa maana ya kushindwa bali kwa maana ya inputs)

Kwenye mifanoa anayoitumia mtume Paulo kuelezea dhana ya utumishi utagundua anarejelea kazi ngumu – askari jeshi, mwanamichezo, mkulima, mjenzi na mchungaji wa mifugo (shepherd). Hizi kazi hazina mwonekano wa ulaini mahali popote. Ni kazi zinazokutaka (demand) uwepo wako wa kimwili, nguvu zako, hisia na muda wako wote. Namna hii ya kazi inataka akili iwepo "mchezoni" muda wote. Ukifumba macho kidogo, umepoteza! Umewahi kumuwaza mwanamichezo anasinzia wakati wa mechi? Haiwezekani.

Mpendwa wangu, ingia kwenye huduma hali ukijua ni kazi inayotaka ugangamale. Kati ya mambo yatakayokuletea sonona, msongo wa mawazo, na hali ya kuchanganyikiwa ni kujidanganya kuwa huduma ni sehemu ya ulaini, kama unateleza vile. Utachanganyikiwa! Kuna mithali kweye semi za

Kiswahili, "Ukitaka kuruka, sharti uagane na nyonga!" Ninafikiri ndivyo ilivyo kwenye kazi ya Mungu.

Ninaposema kazi ya Mungu ni ngumu simaanishi utashindwa bali ninamaanisha itataka kila kitu chako… itakudai pakubwa!

iii. Kazi yenye matokeo ya umilele (With eternity implications)

Kazi ya Mungu haishii hapa. Kimsingi, umilele wa watu wote duniani unategemea utendaji wako wa kazi ya Mungu. Unakumbuka mfano wa Bwana Yesu kumuhusu yule tajiri na maombi yake kwa baba Ibrahimu?

*"Akasema, Basi, baba, nakuomba, umtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akasema,* ***Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao.*** *Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu.* ***Akamwambia, Wasipowasikia Musa na***

***manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu.”*** **Luka 16:27-31**

Musa na manabii inaweza kumaanisha Maandiko Matakatifu (Torati na Unabii). Pia inaweza kumaanisha watumishi wahudumuo kwenye kizazi hicho na nyakati husika. Umilele wa watu wa eneo fulani na watu wa zama fulani unategemea sana watumishi waliopo.

Kazi hii ya Mungu inatafsiri pana ya umilele na hatima za maisha ya watu wote duniani.

Zaidi ya yote, kazi hii ina tafsiri pana ya umilele kwa mtumishi husika. Hii si kazi utakayolipwa, kupandishwa cheo, au kutazamwa mwisho wa mwezi au mwaka au nyakati fulani tu. Nitakuonyesha hili kwenye kipengele cha thawabu.

iv. Kazi ya Dhabihu – toa unachokipenda, toa vipaumbele, toa kwa ajili ya wengine.

Ninapenda kusema **“dhabihu ndiyo jina la mchezo!”** kama ulikuwa hufahamu. Hii kazi itataka kila kitu… itadai kila kitu chako. Itaitaka roho yako, nafsi yako na mwili wako… baba yangu wa kiroho, mtumishi wa

Mungu, Bishop Goodluck Kyara husema, "Uuzwe kikamilifu kwa Bwana."

Umewahi kusoma kitabu changu kiitwacho **Ajitwike Msalaba wake?** Kinaelezea kwa upana sana kuhusu dhana ya dhabihu kwenye utumishi.

*"Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, **na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate**. Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza; na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona."* Mathayo 16:24-25

Umeona huo mtiririko? Inaanza na kujikana mwenyewe kabla ya mambo yote.

Mara zote Yesu alipowaita watu kwenye utumishi, utagundua aliwaita kutoka kwao wenye (he called them out of themselves). Utoke kwako, uje kwake… uje kwenye kazi yake!

Kazi ya Mungu itataka utoe dhabihu ya vitu unavyovipenda… vipaumbele… matamanio… shauku… vionjo! Kimsingi, dhabihu huchinjwa na kuteketezwa. Kiashiria ya kwamba dhabihu imetolewa ni uwepo wa majivu.

Hii ni kazi ya dhabihu. Kama bado wewe umejaa sana ndani mwako (you are full of yourself) kazi hii itakushinda na itakuwa kwazo kubwa. Mungu akusaidie uwe na mtazamo huu kwa jina la Yesu Kristo.

v. Kazi ya thawabu

Mifano yote anayoitumia mtume Paulo kuelezea kazi ya Mungu huwa imeambatanishwa ni hali ya thawabu. Mungu siyo mtuikishaji dhalimu.

*"...kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, **na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.**"* Waebrania 11:6b

*"Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho."* Wagalati 6:9

Ninapozungumza na wachungaji vijana wenzangu, huwa ninapenda sana kuwatia moja kwenye eneo la thawabu kwa kutumia swali la Petro na jibu la Bwana Yesu.

*"Petro akaanza kumwambia, Tazama, **sisi tumeacha vyote tukakufuata wewe**. Yesu akasema, Amin, nawaambieni, **Hakuna mtu aliyeacha** nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au*

*watoto, au mashamba,* ***kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili****, ila* ***atapewa mara mia sasa wakati huu****, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia;* ***na katika ulimwengu ujao uzima wa milele.****"* Marko 10:28-30

Umeona swali la Petro hapo juu… tumeacha vyote! Hayakuwa maneno matupu tu. Alimaanisha alichokisema. Aliacha biashara ya uvuvi wa samaki na alicha mfumo wake wa siku kwa siku wa maisha akaanza kuambatana na Yesu. Kisha Bwana Yesu anaanza kwa kujengea hapo kwenye dhana ya kuacha vyote… mpendwa, hakuna pungufu ya hilo. Kwenye kazi hii kuna kuacha vyote.

Unaona Bwana Yesu anaelezea sababu ya kuacha vyote: **kwa jili yangu na kwa ajili ya injili**. Hio ndiyo unapaswa kuwa msukumo wako wa ndani. Unampenda sana Bwana Yesu na kazi yake kiasi cha kuwa tayari kuacha vyote kwa ajili hiyo. Ni vyema kuchunguza sana nia ya ndani. Ni kwa ajili ya nini nimeacha vyote.

Nimejifunza mapema jambo hili la kuchunguza nia ya ndani. Kwa sababu Mungu anaitwa "Baba aonaye sirini!" Inawezekana watu wanaonizunguka wasijue nia yangu. Yuko Mungu aichunguzaye mioyo na kuvijaribu viuno. Yeye anajua kwa uhakika nia yako.

Bwana Yesu mwenyewe anaeleza ya kwamba matokeo yote: … thawabu yote itapatikana kwenye ulimwengu huu wa sasa  wakati huu. Kisha ulimwengu ujao – wa umilele! Hiyo ni kusema, huyu Mungu wetu hutoa thawabu.

Mtumishi kijana, usiwe mnyonge. Mungu wetu si dhalimu. Mungu wetu hutoa thwabu. Uwe na mtazamo huo ndani yako. Usikae kama vile umejiandikisha kwenye orodha ya watu wanyonge na wakosaji. Usikae kama vile utumishi ni kifungo cha maisha au hukumu ya milele. Utapokea thawabu hapa na mbinguni; sasa na milele mtawalia!

vi. Kazi ya heshima na hadhi

Mtu pekee anayeshughulika na roho, ambaye ndiye mwanadamu halisi, ni mtumishi wa Mungu. Mtu pekee

ameajiriwa na Mungu – anapokea malekezo ya kazi na kuwajibishwa na Mungu, ni mtumishi. Mtu pekee anayepokea rasilimali, ulinzi, uwezesho kutoka kwa Mungu, ni mtumishi. Hii si ni kazi ya hadhi kubwa?

## MAANDALIZI YA KIWITO

Usiingie kumtumikia Mungu kwenye daraja hili mpaka uwe na uhakika amekuita. Kwa sababu ya dhabihu na mapito yanayoambatana na kazi hii, kama huna uhakika kwamba umeitwa na Mungu… kazi itakuwa ya kuchosha sana.

Kinyume chake, yeyote mwenye uhakika ya kwamba ameitwa, chochote kinachoendelea na/au kitachoendelea kitakuwa ni sehemu ya safari inayovutia (adventorous).

Kuna namna kadhaa za kimaandiko ambazo Mungu huwaita watu wake kwenye utumishi.

Mk 3:13-14 SUV, *"[13] Akapanda mlimani, **akawaita aliowataka mwenyewe**; wakamwendea. [14] Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri,"*

Ebr 5:4 SUV, *"[4] Na hapana mtu **ajitwaliaye mwenyewe heshima hii**, **ila yeye aitwaye na Mungu, kama vile Haruni.**"*

Wito kutokakwa Mungu ndiyo utakusababisha kuinuka kila usiku kuomba; kuamka alfajiri na mapema kujiandaa; kuwasili ofisini mapema; kuwapenda watu wote mpaka wanaokuumiza na kukupinga. Wito ndiyo utakusukuma kukesha, kusoma, kuandika… kulia pamoja na waliao, kufurahi pamoja na wanaofurahi. Kuwaona masikini katika dhiki yao. Kuona uzuri ndani ya uchafu wa watu. Kuona mbegu ya kiungu ndani ya makosa. Ni kazi ya wito tu.

Huu utumishi huja na mambo mengi kiasi kwamba wachungaji wengine, kwa kufikiria hushauri watoto wao au watu wawapendao kutoingia kwenye utumishi.

*"Utumishi (uchungaji) siyo kazi ambayo ninaweza kumshauri hata adui yangu aichague."* Rev. Harrison Ayintete

Kimsingi hii ni kazi ya WITO tu... kuna details nyingi zinaambatana nayo.

Nimeandika kitabu kizima kuhusiana na mada ya wito **"Nasikia Kuitwa"**. Kipate ukisome, utasaidika pakubwa.

## MAANDALIZI YA KIMAONO

Mungu anapokuita kwenye utumishi pia hukupa ramani ya namna ya kuuendea wito. Unapaswa kuijua ramani ya uelekeo wa utumishi. Inawezekana usiyajue mambo yote kwa wakati mmoja lakini unapaswa kujua mambo mengi ya kiuelekeo. Ni hatari sana kuinuka kwenda kwenye safari ambayo huijui.

*"Pasipo maono, watu huacha kujizuia;*

*Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria."* Mithali 29:18

Jambo hili la kimaono nimelifafanua kwa upana sana kwenye vitabu kadhaa nilivyoandika. Ninakushauri ulivisome ili kupana kina cha uelewa: **1). Iandike Njozi, 2). Maono Haya Makubwa** na **3). Ninasikia Kuitwa**.

Kwa faida ya fundisho kwenye kitabu hiki, kwa ushahidi mwingi kwenye Maandiko Mtakatifu na nje ya maandiko utagundua kuna watu waliingia kwenye wito bila kuwa na maandalizi haya ya kiwito. Lilikuwa ni jambo gumu sana kwao.

Kuna watu huingia kwenye kazi ya Mungu kwa sababu hawana jambo jingine lolote la maana la kufanya; wengine huwa wameambiwa na watu kwamba wao ni watumishi; wengine ni kwa sababu za uchungu (wameumizwa na viongozi wao au wamejikwaa kwa viongozi wao); wengine ni wimbi la juu la kihisia limewachukua (emotional highs).

Sababu zozote za wito kuingia kwenye kazi ya Mungu ambazo si kuitwa na Mungu ni kosa la kiufundi. Baadaye litakuja kukugharimu. Kwa hiyo, kabla haujatokeza hadharani na kuanza kutenda huduma hakikisha umeitwa na umemuitikia Mungu.

Si umeona neno la Mungu limesema heshima hii haujitwalii tu mwenyewe… hapa anakugawia Mungu kama alivyofanya kwa Haruni.

Kwenye swala la maono, kuna maeneo mawili makubwa ambayo unapaswa kuyatambua. Nitatumia mfano wa ujenzi wa hemani ya kukutania ili kuifafanua dhana hii pana kwa lugha na mfano rahisi.

1. Ramani ya kazi mpya kabisa - kanisa, huduma, mission, movement, taasisi mpya. Kundi hili ni watu walioitwa kuanza kazi mpya.

*"BWANA* ***akamwambia Musa, Njoo huku juu kwangu mlimani, uwe huku; nami nitakupa mbao za mawe na ile sheria na hiyo amri niliyoiandika ili uwafundishe****. 13Musa akaondoka na Yoshua, mtumishi wake, Musa akapanda mlimani kwa Mungu. 14Akawaambia hao wazee, Tungojeeni hapa, mpaka tutakaporudi kwenu; na tazameni, Haruni na Huri wapo pamoja nanyi; kila mtu aliye na neno na awaendee. 15****Musa akapanda mlimani, lile wingu likaufunikiza mlima****. 16Na huo utukufu wa BWANA ukakaa juu ya mlima wa Sinai;* ***lile wingu likaufunikiza siku sita; na siku ya saba akamwita Musa toka kati ya lile wingu****. 17Na kuonekana kwake ule utukufu wa BWANA kulikuwa kama moto uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. 18****Musa akaingia ndani ya lile wingu, akapanda mlimani; Musa akawa humo katika ule mlima siku arobaini, mchana na usiku.****"* Kutoka 24:12-18

*"Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao. **Sawasawa na haya yote nikuonyeshayo**, mfano wa maskani, **na mfano wa vyombo vyake vyote, ndivyo mtakavyovifanya**."* Kutoka 25:8-9

*"Nawe angalia ya kwamba uvifanye **kama mfano wake, ulioonyeshwa mlimani.**"* Kutoka 25:40

*"Ni hivyo utakavyowatendea Haruni na wanawe, **sawasawa na hayo yote niliyokuagiza**; utawaweka kwa kazi takatifu siku saba."* Kutoka 29:35

Hawa ni watu ambao kwa mamlaka huru inayojitegemea ya Mungu mwenyewe (sovereignty) huamua kuwachagua na kuwakabidhi "ramani" ya kazi mpya hapa duniani. Huwaita kutoka miongoni mwa watu na huwaita kibinafsi sana. Ukiyachunguza maandiko utagundua huwa wanabaguliwa… wanawekwa pembeni… wanatengwa!

Kuna sauti, kuna malekezo, kuna maneno, kuna neema, kuna mzigo wa upekee na utofuati huwekewa ndani mwao ili waweze kuliendea jukumu kubwa lililoko mbele yao.

Kwa sababu ya aina ya jukumu la kimaono, watu hawa pia hupewa kiasi fulani cha neema, uwezo, ufahamu, muono, namna ya kuyachukulia mambo, namna ya kuwaelewa na kuchukuliana na watu – hali ya ubaba/ulezi. Nimekuja kugundua, ni watu wa peke yao tu.

Unaona Musa alikuwa na makundi ya wasaidizi wake. Kulikuwa na kundi kubwa la wazee, kisha kulikuwa na Haruni na Huri, na hatimaye kulikuwa na Yoshua, mtumishi wake. Unaona kwa kadiri alivyokuwa akiendelea mbele ndivyo alivyokuwa anawaacha chini. Kwa kadiri anavyopanda mlima, wao wanabakia chini. Mpaka mahali ambapo aliitwa kwenye wingu ambamo alikaa siku arobaini, mchana na usiku.

Kwa taarifa yako, hili ni kundi la watu wachache kiuwiano (relatively). Musa ni mmoja ikilinganishwa na idadi ya watendakazi kwenye maono hayo ya ujenzi wa hema ya kukutania.

Kwa hiyo, kama wewe umeitwa kwa muundo huu. Hakikisha unaelewa upana na kina cha jukumu lako ili

uje uwafundishe na kuwalekeza wengine wote wataokuja na kutenda kazi chini ya uangalizi wako.

Utagundua ya kwamba kila mara ambapo Musa aliambiwa kuhusu mtendakazi fulani chini yake liambiwa huyo atatenda *"sawasawa na ramani"* aliyoonyeshwa Musa mlimani. Haya ni maneno makubwa sana.

2. Kuwa sehemu ya ramani iliyopo: Kundi hili la pili ni la watu walioitwa kutendakazi kwenye ramani iliyopo tayari. Kazi yao ni kuielewa ramani kubwa na kuelewa jukumu lao "dogo" kwenye ramani kubwa.

Hili ni kundi linajumuisha orodha ya wafuatao:

a) Msaidizi
b) Mwendelezaji
c) Mwongeza thamani

Wacha nikuambatanishie mifano kadhaa hapa ili ikusaidie kuelewa:

*"Nawe umlete Haruni ndugu yako karibu nami, na wanawe pamoja naye, miongoni mwa wana wa Israeli, ili anitumikie katika kazi ya ukuhani. Haruni, na Nadabu, na Abihu, na Eleazari, na Ithamari, wana wa Haruni. 2Nawe utamfanyia Haruni ndugu yako mavazi matakatifu, kwa utukufu na kwa uzuri."* Kutoka 28:1-2

*"Nawe utawaambia* ***watu wote wenye moyo wa hekima, niliowajaza na roho ya hekima wamfanyie Haruni mavazi*** *ili kumtakasa anitumikie katika kazi ya ukuhani. 4Na mavazi watakayoyafanya ni haya; kifuko cha kifuani, na naivera, na joho, na kanzu ya kazi ya urembo; na kilemba, na mshipi; nao watawafanyia Haruni nduguyo, na wanawe, mavazi matakatifu ili anitumikie katika kazi ya ukuhani."* Kutoka 28:3-4

*"BWANA akanena na Musa, na kumwambia,* ***2Angalia, nimemwita kwa jina lake Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila ya Yuda;*** *3nami nimemjaza roho ya Mungu, katika hekima, na maarifa, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina,* ***4ili abuni kazi za ustadi,***

*kuwa fundi wa dhahabu, na wa fedha, na wa shaba, 5na kukata vito kwa kutiwa mahali, na kuchora miti, na kufanya kazi ya ustadi iwayo yote. 6Tena, tazama,* ***nimemchagua, awe pamoja naye, huyo Oholiabu****, mwana wa Ahisamaki, wa kabila ya Dani; nami nimetia hekima katika mioyo ya wote wenye moyo wa hekima,* ***ili wapate kufanya vyote nilivyokuagiza****;"* Kutoka 31:1-6

Ukifutilia simulizi hii utagundua kuna makundi kadhaa ya watu walioitwa kwenda kutumika kwenye yale maono makubwa aliyopewa Musa… ile ramani aliyoonyeshwa mlimani. Na kila aliyeitwa, alikuwa na jukumu mahususi la kufanya ili kuchangia kwenye ujenzi wa ramani kubwa.

Haruni na wana wake- hili ni kundi lilikuwa na jukumu la kiroho… ukuhani. Musa hakupaswa kufanya hivyo. Unaona kuna Bezaleli na Oholiabu – hawa ndiyo wasimamizi wakuu wa mradi wote wa ujenzi. Hawa walikuwa na uwezo wa kiufundi na kitaalamu (technical knowledge). Musa siyo mtu "technical" bali yeye ana ramani tu. Kuna wengine walipaswa kushona mavazi mazuri kwa ajili ya Haruni na wana wake.

Ukiwaona unaweza ukadhani wanatenda jukumu dogo. Kumbe ndivyo ramani kubwa inakamilishwa hapo hatua kwa hatua.

Kiuwiano hawa ni kundi kubwa la watu. Mimi binafsi ninapatikana kwenye kundi hili. Sijaitwa kuanza kanisa au taasisi mpya.

Jukumu lao ni kuisoma na kuielewa vyema ramani kubwa aliyopewa Musa. Pili, wanapaswa kuwa kwenye hali ya mashauriano kwa uendelevu na Musa ili kuelewa zaidi taswira aliyoenyeshwa mlimani. Tatu, ni kutumia vipawa, vipaji, ujuzi na maarifa kuongeza thamani kwenye kipande walichowekwa.

Kimaono ni lazima ujue uko upande gani wa utumishi. Kukosa kujua hilo huleta vurugu ndani ya mtu husika na taaisi unayoitumikia.

Nimeshuhudia watu wakihama kutoka kundi la kwanza kuja kundi la pili na kusema, “sikumwelewa tu Mungu vizuri!” tu sentensi kama, “Sikumsikia Mungu vizuri.”. Nimeona wengine wakifunga makanisa, wakiuza makanisa na mali na kusitisha na uendeshaji mzima wa

kitaasisi. Si jambo la kufurahisha. Mkazo wangu mkubwa hapa ni kufahamu umeitwa kutumika kwenye ngazi ipi kimaono. Mwanzilishi au mfuasi.

# MANDALIZI YA KIMAARIFA

Hos 4:6 SUV, *"[6] Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako."*

Yer 3:15 SUV, *"[15] nami nitawapa ninyi wachungaji wanipendezao moyo wangu, watakaowalisha kwa maarifa na fahamu."*

Zab 78:72 SUV, *"[72] Akawalisha kwa ukamilifu wa moyo wake, Na kuwaongoza kwa busara ya mikono yake."*

Kwa taarifa yako kwenye kazi hii swala la kujiongezea maarifa, kujifunza, kusoma na kuchambua siyo *"hobby"* ni sehemu ya maisha. Hii kazi inataka kichwa kinachowaka moto kwa maarifa… kichwa kikali kama wembe! Hii ni kwa sababu kazi ya Mungu inahusisha kila aina ya mtu, kila aina ya maswala (issues).

Utahudumia watu mijini, utahudumia watu vijijini; utahudumua makundi maalum ya watu; utahudumia watu wenye mahitaji ya kipekee kisosholojia; utahudumia maswala ya kiafya, kisiasa, kindoa na familia. Utashughulika na uvunaji wa nafsi na ufuasi; kuhubiri siku za ibada, kubatiza, kufungisha ndoa, kufariji. Utatakiwa kufurahia unapoletewa habari moja ya furaha na unaowahudumia, wakati huo huo kuonyesha kuguswa tokea moyoni na mtu mwingine anayekuletea habari ya huzuni.

Unatakiwa kuwa mshauri nasaha, kuwa baba, kuwa rafiki. Upande mwingine uwe msuluhishi, msimamizi na mfuatiliaji wa karibu wa maendelo ya watu.

Unatakiwa uhudumie kwa njia za kisasa na njia za kimapokeo. Unatakiwa uwe meneja na kiongozi kwa wakati mmoja. Ufahamu namna ya kulea vipawa na kuviachilia. Ni mambo mengi ndani ya kapu moja.

Hata hivyo, kuna mambo yanaainishwa kwenye neno la Mungu kuwa ndiyo kiini cha huduma. Hupaswi kutokuwa nayo.

*"Wale Thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema,* ***Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu*** *na kuhudumu mezani. na* ***sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno.****"*Matendo ya Mitume 6:2,4

Kama neno la Mungu ni biashara basi bidhaa yetu ni neno! Ukiacha kulihudumia neno, umepoteza sauti yako kwenye soko.

Mzee Paulo anamwelekeza mwanae katika imani hii tuishirikiyo ya kwamba jambo ambalo anataka amkute akiendelea kulifanya kwa uendelevu na kwa mkazo wa bidii ni kusoma na kuonya na kufundisha! Hii ni kazi ya kusoma na kufundisha.

*"Hata nitakapokuja,* ***ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha.****"* 1 Timotheo 4:13

Pamoja na vigezo vingine kwa mtu kuwa kiongozi wa kanisa la mahala pamoja, mojawapo ya kigezo ilikuwa ni kujua kufundisha.

*"Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji,* ***ajuaye kufundisha****;"* 1 Timotheo 3:2

Si unajua kufundisha kunahusisha ujuzi (skills). Anaposema ajuaye kufundishaye hamaanishi huduma au karama ya Roho Mtakatifu bali anazungumzia ujuzi.

Hapa ninamaanisha kujua nini cha kufundisha, wakati gani wakufundisha kitu gani, nani afundishwe na kwa namna gani afundishwe… huko ndiko kujua!

- Fundisho (Doctrine) – Ukristo umebeba fundisho gani? Ili mtu aitwe mkristo ni vitu gaani hasa anapaswa kuwa anaviamini? Kuna mfululizo wa kimafundisho ninaandika unaitwa kuitambua imani yetu ambao ninazungumzia kwa kina imani yetu ndani ya Kristo inafananaje. Hapa ninazungumzia sana Maandiko Mtakatifu yaani, Biblia.
- Ufunuo – Hapa ninazungumzia maneno yaliyohusishwa, na kuvuviwa na Roho wa Mungu kutoka kwenye Maandiko Matakatifu kuja kuyahudumia maisha ya watu wa zama za leo. Kwa wale wanatumia lugha nyinginezo watailewa neno la Kiyunani "Rhema"

Ushauri kutoka meza ya mchungaji:

- Jiandikishe kwenye taasisi rasmi za kielimu – Mtumishi, usikae bila kujifunza.
- Shiriki mafunzo/warsha/makOngamano ya kimafundisho/kielimu.
- Shiriki kozi fupi za kujenga uwezo.

Kama unafikiri hayo ni gharama na kufanya mambo yawe magumu (complicated) basi, endelea kutumika ukiwa kwenye hali ya ujinga… uone ujinga una tija kiasi gani kwenye kazi hii ya ufalme.

Habari mbaya ni kwamba, ukikataa maarifa, Mungu anakukataa wewe usiwe kuhani kwake.

## MAANDALIZI YA KIMWILI

Nitaambatanisha dondoo tu zitakazo kufaa kwenye maandalizi ya kwimili. Hapa ninamaanisha mambo ya kiutaratibu ambayo yasipotazamwa yanaweza kuisumbua kazi ya Mungu ambayo umeainiwa kuitenda.

a) Tambua katiba ya taasisi unayofanya nayo kazi na uiheshimu na kuilinda
b) Tambua miongozo ya kitaasisi na uiheshimu
c) Tambua muundo wa kiungozi, mamlaka na mahusiano
d) Tambua utamaduni wa kitaasisi
e) Tambua unaenda kutumika eneo gani la kijiografia – wekeza muda kufahamu demografia.
f) Tambua mkono wako wa nguvu kwenye utumishi na uwekeze huko.
g) Husiana na kuwasiliana na watu wote vyema – kwa mipaka yenye afya.

Kwa ujumla wake, haya yatakusaidia kwanza wewe mwenyewe usijivuruge, na kwa upande wa pili usiwavuruge wengine. Kwa mfano, taasisi unayotokea

inaweza kuwa na utaratibu wa kuwasiliana kwa urasmi kila baada ya mwezi halafu hujui au unapuuza – wewe ni msumbufu na muasi. Usisumbue watu kisha ukaanza kudhani hiyo nayo ni vita katika ulimwengu wa roho kuipinga huduma na wito ulionao.

Usipojua utamaduni wa taasisi unayotokea basi kila mara utajikuta unacheza nje ya mdundo ambalo si jambo la afya kwa yeyote – wewe, watu unaowahudumia, taasisi unayotokea na mwili wa Kristo (ufalme mpana wa Mungu) kwa ujumla wake.

**Kuhusu Mwandishi:**
Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**



NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

**Ratiba za Ibada**

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
+255 754 917 764